


SAFARI YA KUTAFUTA MAKAO AMERIKA

Unapofika Amerika, ni vizuri kufahamu kuwa makao yako haitakuwa kama ile yenye uliona ku television, katika film, ao ku matangazo. Batu mingi Amerika banaikala ku nyumba ao vyumba ya kawaida ao vidogo. Ni vizuri pia kujua kama kwa sasa makao Amerika iko chache, na haitoshi kwa batu benye kutafuta nyumba—na hasa nyumba za bei muzuri.



KUELEWA MAKAO YAKO YA KWANZA AMERIKA




Wakati ya kufika Amerika unaweza kupewa makao ya muda kama vile hoteli, chumba ku université, ao nyumba yenye vyombo ndani. Mara nyingi ile nyumba ya muda iko fasi ya karibu na ina vifaa kama vile vyombo vya mafika, vifaa vya kufua nguo, na mambo ingine. Unaweza kuikala ku ile nyumba kwa muda wa mainga ao myezi mpaka wakati utapata makao ya muda murefu.

Kama nyumba yako ya kwanza ni ya muda mufupi ao ya muda murefu kidogo, wewe na familia yako mutakaribishwa na chakula muzuri na ndani ya mafika kutakuwa chakula ya kuanzia maisha. Pia ndani ya nyumba kutakuwa vifaa ya usafi binafsi na vifaa ya kusafisha nyumba.



KUPATA MAKAO YA MUDA MUREFU



Mara nyingi bei ya nyumba Amerika iko juu sana, kwa hiyo inaweza kuwa vigumu kupata fasi ya kuikala yenye iko salama, safi na ya bei muzuri. Wakati wa kutafuta makao ya kudumu Amerika, ni lazima kulinganisha kitumaini na vile vitu vilipo. Ni lazima fasi ya kuikala, ukubwa, urahisi na uzuri ya makao vyote vilingane na mapato yako ya kila mwezi. Fasi yote mu inchi, malipo ya nyumba ndiyo itakuwa sehemu kubwa zaidi ya mapato yako ya kila mwezi.

Utakapofika Amerika utakuwa na mapato kidogo. Inawezekana nyumba ya kudumu yenye utapata haitakuwa sawasawa na matumaini yako yote. Kama ulikuwa katika makao ya muda mufupi kwa inga za kwanza Amerika kama vile hoteli ao Airbnb, nyumba ya kudumu inaweza kuwa haiko muzuri kama ile ya muda mufupi.

Kwa wakati, unaweza kupata nyumba bora kufuatana na kuongezeka kwa mapato yako, alama ya mkopo, na akiba yako. Kufahamu utaratibu wa kutafuta nyumba katika mahali ya makao yako inaweza kusaidia kupata nyumba yenye kulingana na mahitaji yako.

Kama unaona magumu kupata nyumba ya bei muzuri Amerika, haiko weye tu. Kuna shida ya ukosefu wa nyumba za bei muzuri katika majimbo yote 50, na shida hiyo siyo ya wakimbizi na wageni wengine Amerika peke yao bali ni ya raia wa Amerika pia.





KUTAMBUA MAHITAJI YAKO YA NYUMBA

Mbele ya kuanza kutafuta nyumba, unapashwa kutambua mahitaji yako ya makao. Ni **lazima** ujuwe mambo haya wakati wa kutafuta nyumba. Kwa kujisaidia kutambua mahitaji hayo:



- Angalia budget yako ili kujua pesa ngapi unaweza kulipa kodi ya nyumba, na kuhakikisha pesa ngapi utapashwa kulipa zaidi ya kodi. Ukikodi nyumba, angalia kama kuna malipo zaidi ya kodi kila mwezi, kama vile vifaa vya nyumbani na assurance.
- Fikiria ukubwa wa nyumba yenye unahitaji, pamoja na kuhesabu vyumba na fasi ya kuweka motokari yako



- Jiulize kama fasi kwenye unaikala inatimiza mahitaji ya familia yako. Kwa mfano, angalia safari ya kwenda ku kazi na ku masomo, na kama kuna njia ya usafiri wa watu wote. Kama wewe au mtu mwingine katika familia yako ana magumu ya ulema, hakikisha kuwa nyumba yako itatimiza mahitaji hayo.
- Pima usalama wa fasi kwenyi unaikala na uhakikishe kuwa mambo ya kusaidia iko karibu wakati wa hatari kama vile polisi na hospitali au kliniki.



Kila familia iko mbalimbali na zingine na ina mahitaji mbalimbali. Hii maswali inaweza kukusaidia kutambua mahitaji yako au ya familia yako na kuelewa nyumba gani iko bora.

Cultural Orientation Resource Exchange

For more information, visit Settle In at settlein.org.